OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

SIMU:0753944697(Mkuu wa shule)

0786971327(Mkuu wa shule)

0621277309/0768699618(Makamu wa shule)

SHULE YA SEKONDARI MKOLE,

S.L.P 66,

NAMANYERE-NKASI.

KUMB.NA/NKS/SEC/MKL/F.I/2020

MWANAFUNZI----------

S.L.P----------

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKOLE ILIPO WILAYA YA NKASI MWAKA 2020

1.0. Ninayo furaha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule hii kwa mwaka 2020.

1.1. MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya Sekondari Mkole ipo umbali wa kilomita 16 kasikazini mwa mji wa Namanyere.Kokote utakakopandia gari wambie wahusika wakushushie SEKONDARI Usafiri wa **BASI** kutoka mjini Namanyere unapatikana katika kituo cha mabasi cha stendi kuu (Mkuyuni) nauli ni Tsh 2,000/=

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2020 unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia tarehe**11/01/2020** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2020**

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1.SARE ZA SHULE

A. WASICHANA

i. Sketi ya kaki moja(1) na nyeusi moja(1) zenye linda moja pana mbele na nyuma na malinda madogomadogo pembeni. **Sketi hizo lazima ziwe ndefu mpaka kwenye kisigino cha mguu tofauti na hapo atashona upya.**

ii. Mashati mawili meupe mikono mifupi aina ya **TOMATO**

iii Viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi**(viatu aina ya bajaji havitakubaliwa)**

iv. Soksi nyeupe jozi mbili

v. Kanga jozi moja kwa ajili ya kujifunga anapokwenda bafuni kuoga**(NI MUHIMU SANA)**

vi. Sweta la zambarau.

Scanned with CamScanner

vii. Shamba dress **(Magauni ya rangi ya damu ya mzee jozi mbili kwa ajili ya kushindia) Haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani (MARUFUKU)**

viii. Fulana rangi ya damu ya mzee **NIACHE NISOME**.Zinapatikana Shuleni kwa Tsh.10,000/=

ix.Nguo za michezo: Fulana rangi ya blue na **truck suit ya blue** pamoja na raba(viatu)

x. Leso moja au zaidi ya moja kadri ya uwezo

B.WAVULANA

i. Suruali ya kaki moja(1) na nyeusi moja(1)***SURUALI HIZI ZIWE ZA KUSHONWA ZA KUTUNGUA HAZITAKIWI ZIWE NA MARINDA MAWILI KILA UPANDE NA ZIWE NA MIFUKO MIWILI NYUMA SURUALI AINA YA MODO HAITAKIWI NA KUVALIA CHINI YA MAKALIO NI MARUFUKU.***

ii. Mashati mawili meupe mikono mifupi aina ya **TOMATO**

iii. Viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga kwa kamba

iv. Soksi nyeusi jozi mbili

v. Sweta la zambarau

vi. Fulana ya blue **na truck suit ya blue** ambayo ndiyo mavazi ya kushindia.

NB. Fulana ya blue ni muhimu sana kuja nayo kwani wakati akiwa shuleni haruhusiwi kuvaa mavazi ya nyumbani.

vii. Nguo za michezo: Bukta ya blue au nyekundu,fulana ya blue na raba(viatu)

2:2. VIFAA VYA DARASANI

i. Daftari kubwa kumi na mbili(12) QUIRE 2

ii. Mkebe(Mathematical set) **wenye ramani ya dunia juu**

iii. Kamusi ya Kiingereza na Kiswahili(**CONCISE DICTIONARY)**

iv. Saa ya mkononi

v. Leso moja au zaidi ya moja kadri ya uwezo

2.3. Shule yetu ina Hostel kwa ajili ya Wasichana,hivyo kwa wanaoishi Hostel(wasichana wote)watatakiwa kuwa na mahitaji yafuatayo.

i. Godoro la futi $2^{1/2}$x6(mbili na nusu kwa sita)

ii. Mashuka mawili(2)ya rangi ya pinki AU blue rangi tofauti na hizo hazitakiwi Hostel

iii. Mto na foronya zake za pink au blue

iv. Blanketi moja

iv. Chandarua

v. Sahani,Bakuri,Kijiko na Kikombe kwa ajili ya kulia chakula

vi. Tranka(sanduku(1)imara kwa ajili ya kutunzia mali zake

vii. Ndoo moja kwa ajili ya kuogea na kufulia dumu la lita tano jipya kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.

Scanned with CamScanner

2.4 MCHANGO WA CHAKULA

Kwa wale wanaokaokaa Hostel(**wasichana**) au WAVULANA watakaotaka kula shuleni watatakiwa kuleta

i. Fedha ya upishi **Tsh.60, 000/**=kwa mwaka au **Tsh.30, 000/**=kwa nusu mwaka Mwanafunzi wa Hostel atapokelewa iwapo amelipia mwaka au nusu Mwaka.

ii. Mahindi sado 50 kwa mwaka au sado 25 kwa nusu mwaka

iii. Maharage sado 15 kwa mwaka au sado 4 za kuanzia

ANGALIZO. *Mahindi na Maharage vipepetwe na kuchambuliwa vizuri kabla ya kuletwa Shuleni, Mahindi machafu na Maharage yaliyooza hayatapokelewa.*

2.5 USAFI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Mwafunzi atatakiwa kuja na.

i. Mche wa mti mmoja kwa ajili ya kupanda. Mche huo unaweza kuwa wa mbao au matunda

ii. Ufagio kwa ajili ya usafi aina ya CHELEWA na jembe

3.0. MATIBABU

Mzazi utatakiwa kumlipia mwanao BIMA YA AFYA CHF iliyoboreshwa kwa ajili ya matibabu pindi atakapougua akiwa shuleni ambapo serikali imeweka kiwango cha tsh.5, 000/= tu.

3.1 SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana na elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo.

(a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii nzima kwa ujumla ni jambo la LAZIMA.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhihmu

(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni(preparation)

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa

(e) Kufaahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo ya juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa ikiwa nadhifu.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi,cocaine,mirungi,kuberi n.k

Scanned with CamScanner

5. **Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzako**
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera ya taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba ua kusababisha mimba ndani au nje ya shule
10. Kutoa mimba
11. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. **Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi**

KARIBU SANA MKOLE SEKONDARI

BUDODI P.D

MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
DATE.....
Box 66-NKASI
MKOLE SECONDARY SCHOOL

Scanned with CamScanner